**ECHO NETWORK AFRICA LIMITED ("Kampuni")**

**KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA ZA KAMPUNI KATIKA MWAKA WA 2023 ULIOFANYIKA KUPITIA MTANDAO JUMATANO, TAREHE 16 AGOSTI 2023 SAA 4:00 ASUBUHI.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Waliohudhuria** | Dkt. Nyambura Koigi | | Mwenyekiti |
| | Bi. Ursula Sore- Bahati | - | Mwenyekiti |
| | Dkt. Jennifer Nkuene Riria | - | Afisa Mkuu Mtendaji |
| | Bi. Selinah Jepkoech Kibogy-Kandie | - | Mkurugenzi |
| | Bi. Jeniffer Nyambura | | Mkurugenzi |
| | Bi. Elizabeth Achola Mang'eni | - | Mkurugenzi |
| | Bi. Joyner Okonjo | - | Mkurugenzi |
| | Bi. Verity Mbaka Nyagah | - | Mkurugenzi |
| **Wanachama** | Watu 58 | | |
| **Waliohudhuria** | Wasimamizi na Wafanyakazi | | Echo Network Africa Limited |
| | Bi. Winnie Jumba | | Katibu wa Kampuni |
| | Bw. Elvis Ogeto | - | RSM Eastern Africa (Mkaguzi wa Hesabu) |

**KUMB 1/2023 TAARIFA YA MAKARIBISHO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wanachama wote kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka na kisha kuwatambulisha Wakurugenzi wa Bodi, Mkaguzi wa Hesabu, Katibu wa Kampuni na Wasimamizi Wakuu waliokuwepo hapo na waliohudhuria kupitia mtandao.

**KUMB 2/2023 TANGAZO LA KUTHIBITISHA IDADI INAYOAFIKI MKUTANO**

Katibu wa Kampuni alisoma tangazo la kuitisha mkutano na akathibitisha kuwa mkutano ulikuwa na idadi ya watu ya kutosha kutekeleza shughuli za Mkutano Mkuu wa Mwaka.

Marekebisho kwenye ajenda ya kufuta kipengele cha 7 (b) yaliangaziwa.

Mwenyekiti alitangaza kuwa mkutano umefikisha idadi ya watu ipasavyo.

**KUMN 3/2023 KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA ULIOFANYIKA JUMANNE TAREHE 23 SEPTEMBA 2022**

Kwa pendekezo la Victoria Nagwalla, lililoungwa mkono na Pauline Mumbua, kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Mwaka (AGM) uliofanyika tarehe 23 Septemba 2022 ziliwasilishwa na kuthibitishwa kama rekodi ya kweli ya shughuli za mkutano huo.

**KUMB 4/2023 RIPOTI YA MWENYEKITI**

Taarifa ya Mwenyekiti iliwasilishwa na muhtasari wa mambo muhimu kutoka katika ripoti hiyo ulibainishwa kama ifuatavyo:-

a) **Hali ya biashara**

Mwaka wa 2022, Kenya ilikabiliwa na changamoto sugu ambazo ziliathiri vibaya jamii ya Kenya na haswa: wasichana, vijana, wanawake wenye ulemavu na wale kutoka kwa jamii zilizotengwa. Zaidi ya hayo, uchaguzi mkuu wa 2022 ulisababisha tofauti, mfadhaiko miongoni mwa wananchi na uchumi kudorora. Hali hii ilifanywa kuwa mbaya zaidi kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi; vipindi virefu vya ukame, vita vya Urusi na Ukraine, na athari za muda mrefu za Covid-19.

Pato la Taifa la Kenya (GDP) lilipungua hadi 5.5% mwaka 2022 kutoka 7.5% mwaka wa 2021 kutokana na ukame wa muda mrefu, kuongezeka kwa bei za bidhaa na hali ngumu ya kifedha duniani. Licha ya changamoto mbalimbali, Kampuni iliendelea kuchochea mikakati yake ambayo ilijumuisha: fedha za kukopa na kulipa, utoaji wa

vifurushi vya hadhi kwa wasichana shuleni na kufundisha stadi za maisha na ushauri wa STEM (Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati) kutoka kwa mifano ya kuigwa ya Kaunti za Narok na Meru.

b) **Mafanikio ya 2022**

Baadhi ya mafanikio muhimu yanajumuisha:

- Mpango mkakati wa 2018 -2022 ulihitimishwa kwa ufanisi mnamo Desemba 2022. Aidha, mafunzo yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mkakati uliohitimishwa ambao ulikuwa msingi wa kutunga Mpango Mkakati wa 2023-2027. Mpango huo unajumuisha dhamira ya ENA ya kupanua utoaji wa mikakati yake kote nchini Kenya na kanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Hatua za ENA za mwaka wa 2022 ziligusa maisha ya wasichana wengi, wanawake, na familia huko Homabay kupitia ufugaji wa samaki pamoja na kufanya kazi na shule ya mashinani huko Meru kushughulikia uhifadhi wa wasichana shuleni.
- ENA ilifanikiwa kuandaa matukio ya ngazi ya juu ya utetezi na kuleta pamoja Serikali, washirika wa maendeleo, asasi za kiraia na wadau wengine wanaohusika katika kupigania uundaji wa jamii bora.

c) **Utawala**

- Bodi iliendelea kuzingatia kanuni za utawala bora katika shughuli zake zote na taasisi. Ilibainishwa kuwa Bodi ya ENA ilihudumu kwa miaka mitatu kwa mzunguko. Wanachama walifahamishwa kuwa Bi. Selinah Kandie atastaafu kutoka kwa Bodi wakati wa mkutano huo. Mwenyekiti alimshukuru Selinah kwa kujitolea kwake kwa Kampuni.
- Kuanzia 2023, wanachama wawili wanaume wangetambulishwa kwa Bodi kwani ENA inafuata Katiba kuhusu kanuni za Jinsia.

Baadaye, ripoti ya Mwenyekiti ilipitishwa kwa pendekezo la Esther Okeiga na kuungwa mkono na Virginia Njeri.

K**UMB 5/2023** **RIPOTI YA MKURUGENZI MKUU WA KAMPUNI**

Mkurugenzi Mkuu Mtendaji aliwashukuru wote waliohudhuria mkutano huo na kisha kusoma mambo muhimu kutoka kwa ripoti yake.

Muhtasari mambo muhimu kutoka kwa ripoti yake yalibainika kama ifuatavyo: -

Mkurugenzi Mkuu Mtendaji alitoa ripoti kuwa ENA iliendelea kufanya kazi na Washirika wa sekta binafsi, mashirika ya serikali, watu binafsi na mashirika ambayo yalishiriki maono ya kuona ulimwengu unabadilika na kuwa jamii yenye haki na yenye usawa.

Aliangazia mafanikio yafuatayo:-

- Kupitia "Kampeni ya Chagua Mama", wanawake 184 walipewa mafunzo ya "Kukimbia ili Kushinda". Watano kati ya wanawake hao walikuwa wanawake wenye ulemavu ilhali kumi na sita walikuwa wanawake vijana. ENA ilifanikiwa kuwa na magavana 7 ikilinganishwa na magavana 3 mwaka wa 2017.
- ENA iliweza kununua vifaa vya kiteknolojia ili kuongeza ufanisi wa ufugaji wa samakai kwa vizimba, uvunaji na uhifadhi, kuongeza ujuzi wa wanawake katika uongezaji thamani na uuzaji, kutoa ufikiaji wa Hazina ya Mkopo wa Kuzunguka na kuwezesha uhusiano na vifaa na huduma za serikali katika kaunti ya Homa Bay.
- Wanachama wa vikundi 16 vya wanawake katika kaunti za Marsabit na Samburu walifunzwa kuhusu mseto na uongezaji thamani; kuunda vifaa vya sanaa, ufugaji wa nyuki na mifugo.
- Maeneo yaliyolengwa katika Uongozi wa Wanawake, Ushiriki wa Kisiasa na Utawala yanajumuisha:
    a) Kuongeza idadi ya wagombea wanawake waliojitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uchaguzi mwaka wa 2022, wakiwa 1,773 mwaka wa 2022 ikilinganishwa na 1,259 mwaka wa 2017 na 971 mwaka wa 2013.
    b) Kuongezeka kwa ufahamu wa manufaa na haja ya uongozi unaojumuisha jinsia zote nchini Kenya kupitia "Kampeni ya Chagua Mama".

c) Kuongezeka kwa ufadhili wa mikakati ya kisiasa kutoka chini ya milioni 1 hadi zaidi ya Shilingi milioni 50 na kupanua usaidizi kutoka kwa mshirika mmoja hadi wanne wa maendeleo.
d) Iliunda muungano wa mabingwa wa jinsia zaidi ya 852 ili kuendelea kusaidia na kutetea na kulinda faida za kijinsia zilizoelezwa katika Katiba ya 2010.
e) Kuchapishwa na kusambazwa angalau Vitabu na Vijitabu Kumi ili kujenga msingi wa maarifa wa ENA kuhusu Uongozi wa Wanawake.
f) Kuongezeka kwa viwango vya wasifu wa ENA na sifa ya kimataifa, kikanda na nchini kufuatia utambuzi wa ENA na Apolitical Foundation mwaka wa 2022 kama mojawapo ya mashirika 28 yenye ubunifu zaidi ya kuangaziwa duniani kote.

- Kituo cha Programu cha Girls Excel kilichangia kuongeza ufahamu na utetezi kuhusu uzuiaji wa mazoea hatari kama vile ukeketaji, mimba za utotoni, na ndoa za mapema na za kulazimishwa katika Kaunti ya Narok.
- Mpango wa Tuvuke ulilenga katika kuongeza uwezo wa wanawake watendaji wa amani ili kushiriki katika michakato ya kulinda amani ipasavyo huku wakiimarisha jukumu lao katika kujenga amani na kukuza kuishi pamoja kwa amani katika ngazi ya jamii.
- Kuhusiana na utawala, Mkurugenzi Mkuu Mtendaji alitoa ripoti kwamba Bodi ya ENA ilipatiwa mafunzo ya kujenga uwezo wao katika uongozi, masharti ya utawala wa kimataifa, uwajibikaji na usimamizi.

Baadaye, ripoti ya Mkurugunzi Mkuu Mtendaji ilipitishwa kwa pendekezo la Jane Bundi na kuungwa mkono na Maren Omollo.

**KUMB 6/2023 TAARIFA ZA FEDHA ZA MWAKA ULIOKAMILIKA TAREHE 31 DISEMBA 2022.**

Ripoti ya Wakurugenzi na Wakaguzi pamoja na Taarifa za Fedha za mwaka uliokamilika tarehe 31 Desemba 2022 ziliwasilishwa. Ripoti ya Wakurugenzi ilipitishwa kama ilivyosomwa.

Bw. Elvis Ogeto anayewakilisha Wakaguzi, RSM Eastern African LLP alisoma Ripoti ya Wakaguzi wa Hesabu kwa wanachama.

Mwenyekiti alitaarifu mkutano kuwa wajumbe walipewa nafasi ya kuuliza maswali na kupata ufafanuzi kuhusu taarifa za fedha. Majibu yalitolewa kwa wanachama wote waliouliza maswali na kutaka ufafanuzi.

Kwa pendekezo la Bella Mukwanze na kuungwa mkono na Millicent Agesa, iliamuliwa kuwa Taarifa za Fedha pamoja na Ripoti za Wakurugenzi na Wakaguzi wa Hesabu za mwaka uliokamilika tarehe 31 Desemba 2022 zikubaliwa na kupitishwa.

**KUMB 7/2023 UCHAGUZI WA WAKURUGENZI**

a) Ilibainika kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 44 cha Sheria za Makampuni, Bi. Selinah Kibogy Kandie akiwa amemaliza muhula wake wa miaka miwili, hakustahili kuchaguliwa tena.

b) Ilibainika kuwa kulingana na Kifungu cha 47 cha Sheria ya Makampuni, Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza kuteuliwa kwa Bw. Oliver Waindi kuwa Mkurugenzi wa Kampuni. Mwenyekiti aliendelea kutoa maelezo mafupi ya wasifu wake.

Kwa pendekezo la Caroline Mutethia Mbithuka na kuungwa mkono na Regine Muinde, iliamuliwa kumteua Bw. Oliver Waindi kuwa mkurugenzi wa Kampuni.

**KUMB 8/2023 WAKAGUZI WA HESABU ZA FEDHA**

Kwa pendekezo la Elizabeth Mang'eni, akiungwa mkono na Catherine Ng'ang'a, iliamuliwa kuteuliwa tena kwa Messrs RSM Eastern Africa LLP, ofisini kama Wakaguzi wa Hesabu za Nje wa Kampuni kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 721(2). ) ya Sheria ya Makampuni, 2015. Pia iliamuliwa kuwa Wakurugenzi waidhinishwe kutoa malipo ya Wakaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha unaoliokamilika, kwa mujibu wa Kifungu cha 724 (1) cha Sheria ya Makampuni, 2015.

**KUMB 9/2023 SHUGHULI MAALUM**

a) **Kubadilisha jina la Taasisi, ENA ili lile ENA Foundation**

Kulingana na pendekezo la Polly Ntinyari, lililoungwa mkono na Sheila Odhiambo, iliamuliwa kwamba kupitia azimio maalum, jina la Kampuni libadilishwe kutoka Echo Network Africa Limited hadi Echo Network Africa Foundation na kuachana na matumizi ya neno "Limited" kulingana na idhini ya Msajili wa Makampuni.

b) **Kuanzisha Ofisi ya Nchini Kenya ya ENA**

Kwapendekezo la Agnes Ochieng na kuungwa mkono na Sheila Odhiambo, **iliamuliwa** kwa azimio la kawaida kwamba kuanzisha na kusajili Ofisi ya Nchi ya Kenya kuidhinishwe na kupitishwa na wakurugenzi walio na uwezo wa kufanya mambo yote muhimu ili kutekeleza azimio hili na vitendo vyao vyote kuhusiana na yale yaliyofanywa kabla ya tarehe ya azimio hili uidhinishwa, kupitishwa na kuthibitishwa.

c) **Marekebisho ya Mkataba na Sheria za Kampuni**

Kwa pendekezo la Pauline Mumbua na kuungwa mkono na Bella Mukunza, **liliamuliwa** kupitia azimio maalum la kupitisha marekebisho yafuatayo ya Mkataba na Sheria za Kampuni:-

<u>Mkataba wa Kuunda Kampuni</u>

i. Ili kufuta kifungu cha 1 kabisa na kukibadilisha na:
"Jina la Kampuni ni "Echo Network Africa Foundation"'.
ii. Ili kufuta kifungu cha 3 kabisa na kukibadilisha na:
"Kuchagua na kuteua kwa muda na kwa masharti kama itakavyoona inafaa, kwa mujibu wa masharti ya 3.2 na 3.3 hapo juu, watu wenye ujuzi unaofaa kuwakilisha kampuni, kusimamia na kuendeleza shughuli za ofisi yoyote ya nchi katika kuendeleza malengo ya kampuni na kuteua kwa kila ofisi ya nchi afisa atakayewakilisha maslahi ya kampuni. "
iii. Kujumuisha Kifungu cha 3.33 kwenye kifungu cha 3.26 ili kuepuka urudiaji na kwamba vifungu hivi viwekwe nambari mpya ipasavyo.
iv. Kufuta maneno "na kukopa au kuchangisha pesa" kutoka kwa Kifungu cha 3.28 ili kuepuka urudiaji kwa kuwa hiki kimejumuishwa kwenye kifungu cha 3.26.

<u>Sheria ya Kampuni</u>

Sheria za Kampuni ya ENA zinarekebishwa ili kujumuisha yafuatayo pamoja na kwamba vifungu hivi viwekwe nambari upya ipasavyo:

i. Kurekebisha kifungu cha 1.5. kufafanua "Rais na Afisa Mkuu Mtendaji" kama "Mtu aliyeteuliwa chini ya Kifungu cha 69 kusimamia shughuli za kila siku za Wakfu na ambaye atakuwa Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi."
ii. Ili kuongeza yafuatayo kwa kifungu cha 9:
"Hakuna mwanachama atakayestahiki uwanachama ili anadaiwa pesa fulani na kampuni kutekeleza au kufurahia haki yoyote au marupurupu ya Uanachama au kupiga kura kuhusu jambo lolote au kugombea uchaguzi au kupendekeza Mwanachama mwakilishi yeyote wa Kampuni kwa uchaguzi."
iii. Ili kuingiza kifungu kipya baada ya kifungu cha 9 (nambari 10):
"Mwanachama yeyote akifariki, akiwa hana akili timamu au akitangazwa na mahakama kuwa amefilisika au kampuni ikifilisika kwa lazima au kwa hiari, au kampuni ivunjwe, Mwanachama huyo atakoma kuwa Mwanachama wa Kampuni."
iv. Ili kuingiza kifungu kipya baada ya kifungu cha 10 (nambari 12):
"Hadi itakapoamuliwa vinginevyo na Bodi kwa mujibu wa Kifungu cha 3, uanachama utakuwa wa aina zifuatazo:
a) Wanachama waanzilishi
b) Wanachama wa heshima
c) Wanachama wa kawaida
d) Wanachama washiriki

Bodi, kwa hiari yake, itakuwa na uwezo wa kutoa haki, marupurupu na madeni inapohitajika, panapofaa, inayohusishwa na aina yoyote ya Uanachama. Bodi

pia itakuwa na uwezo wa kubadilisha, kurekebisha au kufuta haki na marupurupu yanayohusishwa na aina yoyote ya uanachama katika Kampuni.

v. Ili kuingiza kifungu kipya baada ya kifungu cha 10 (nambari 13):
"Wanachama waanzilishi ndio waliojiandikisha kwenye sheria ya kampuni na wana haki ya kuwa mwanachama wa kudumu."

vi. Ili kuingiza kifungu kipya baada ya kifungu cha 10 (nambari 14):
"Bodi itakuwa na uwezo wa kuchagua watu ambao wamehudumia kampuni vizuri kwa muda mrefu kwa malengo ya Kampuni kwa uanachama wa heshima kwa masharti ambayo bodi itaonelea yanafaa. Uanachama wa heshima utampa mtu huyo haki ya uanachama wa milele kwa mujibu wa Kifungu cha 9."

vii. Kurekebisha kifungu cha 11 (namba 15) kisomwe kama ifuatavyo:
"Uanachama wa kawaida wa Kampuni utakuwa wazi kwa mtu yeyote, wanawake, vijana wa kike na wanawake wanaoishi na ulemavu na kategoria za ushirika na aina zingine zozote ambazo Bodi inaweza kuamua mara kwa mara;

15.2 Mwanachama lazima awe na zaidi ya miaka 18.

15.2 Mwanawake aliyestahiki, vijana wa kike na wanawake wanaoishi na ulemavu wanaweza kustahiki uanachama.

15.3 Makampuni yaliyojitolea kuendeleza malengo ya Kampuni hili yanaweza kustahiki uanachama.

viii. Ili kuingiza kifungu kipya baada ya kifungu cha 10 (nambari 16):
"Bodi inaweza mara kwa mara, kwa hiari yake, kualika watu binafsi au shirika lolote lililoanzishwa chini sheria ambalo halistahiki kuwa na uanachama chini ya Kifungu cha 11 kuwa mwanachama Mshiriki wa Kampuni. Wanachama washiriki watalipa usajili huo au kutoa mchango wa fedha za Kampuni itakavyoamuliwa na Bodi. Wanachama washiriki hawatakuwa hawezi kupiga kura katika Mkutano Mkuu wowote, lakini wanaweza kuwa na, katika masuala mengine yote, haki na marupurupu na majukumu sawa na wanachama wengine. Bodi pia itakuwa na mamlaka ya kusimamisha au kufuta haki na marupurupu ya mjumbe yeyote baada ya kusikizwa kwa kesi kama hizo zikiletwa mbele yake lakini haitalazimika kutoa sababu yoyote ya uamuzi wake."

ix. Kurekebisha kifungu cha 33 (namba 38) kisomwe kama ifuatavyo:
"Mwanachama anayepiga kura atakuwa na kura moja tu."

x Kurekebisha kifungu cha 55 (namba 60) kisome ifuatavyo: "Bodi itakuwa na mamlaka ya kuidhinisha kuanzisha ofisi ya Nchini katika nchi mbalimbali duniani kwa kuzingatia sheria za nchi hizo mbalimbali."

xi. Ili kurekebisha mada kabla ya kifungu cha 71 (nambari 76) kisome ifuatavyo: "Rais na Afisa Mkuu Mtendaji".

xii. Kurekebisha kifungu cha 71 (namba 76) kisome ifuatavyo: "Wakurugenzi wanaweza mara kwa mara kuteua Rais na Afisa Mkuu Mtendaji au vinginevyo ambaye wakati wote atakuwa wa jinsia ya kike, kwa muda ambao kwa masharti watakayoonelea yanafaa, na kwa kuzingatia masharti ya makubaliano yoyote yaliyofikiwa kwa hali yoyote, anaweza pia kubatilisha uteuzi huo. Mtu aliyeteuliwa akiwa anashikilia wadhifa huo hatastaafu kwa zamu au Mtu aliyeteuliwa wakati akiwa anashikilia wadhifa huo hatalazimika kustaafu kwa zamu au kuzingatiwa katika kuamua zamu au kustaafu kwa Wakurugenzi, lakini atakoma moja kwa moja kuwa Mkurugenzi baada ya kuacha kuteuliwa kuwa Afisa Mkuu Mtendaji."

xiii. Kurekebisha kifungu cha 74 (nambari 79) kisome ifuatavyo: "Wakurugenzi wanaweza kumtwika na kumpa Rais na Afisa Mkuu Mtendaji mamlaka yoyote anayoweza kutekeleza kwa mujibu wa sheria na masharti watakavyoonelea yanafaa, na ama kwa dhamana na au kwa kuweka nje mamlaka yao wenyewe na wanaweza mara kwa mara kubatilisha, kuondoa, kufuta au kubadilisha mamlaka yote au mojawapo kati yao."

xiv. Kurekebisha kifungu cha 75 (nambari 80) kisome ifuatavyo: "Rais na Afisa Mkuu Mtendaji atawajibika kwa usimamizi wa kila siku wa Wakfu na atawajibika kwa kuajiri, utendakazi na nidhamu ya wafanyakazi wote wa kudumu, wa muda na wa vibarua."

xv. Kufuta kifungu cha 76 kabisa "Afisa Mkuu Mtendaji atawakilisha maslahi ya Kampuni katika kusimamia utendakazi na shughuli za ofisi za Nchini"

**Kumb 10/2023 SHUGHULI NYINGINE YOYOTE**

Katibu wa Kampuni alithibitisha kuwa hakuna notisi ya kushughulikia shughuli nyingine yoyote iliyopokelewa.

**MWENYEKITI ALITANGAZA MKUTANO HUO KUFUNGA MAJIRA YA SAA 5:35 ASUBUHI**

Imeidhinishwa tarehe 2024.

**MWENYEKITI:** ……………………………………